OFISI YA RAIS TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA
HALMASHAURI YA WILAYA YA HANANG'

SHULE YA SEKONDARI CHIEF GIDOBAT,
S. L. P 167,
KATESH-HANANG.

……..

KUMB. NA. CGSS/ADM/VOL.1/12/2021
MZAZI/MLEZI WA……
……..
S. L . P …….
…….

YAH: <u>MAAGIZO YA KUJIUNGA NA SHULE YA SEKONDARI CHIEF GIDOBAT WILAYA YA HANANG' MWAKA 2021</u>.

Ninayofuraha kubwa kukuarifu kuwa mwanao amechaguliwa kujiunga na kidato cha kwanza katika shule ya sekondari Chief Gidobat mwaka 2021. Shule ya sekondari Chief Gidobat ipo umbali wa Km. 2.5 Magharibi mwa Mji wa Endasak ulioko Wilaya ya Hanang.

Muhula wa kwanza wa masomo unaanza kuanzia tarehe …….…… na mwanao anapaswa kuripoti shuleni kuanzia siku hiyo na mwisho wa kuripo ni tarehe …….

MAMBO MUHIMU YA KUZINGATIA

Sare za shule:

Ni muhimu ifanane kwa rangi, mishono na ubora wake.

WAVULANA:

- Shati mbili nyeupe aina ya tetron mikono mifupi
- Suruali mbili rangi ya …….mshono wa kawaida marinda mawili
- Sweta rangi ya ……..shingo V.
- Viatu vyeusi vya ngozi jozi moja yenye kamba na visiwe na visigino virefu
- Soksi rangi ya khaki pea mbili
- Mfuko wa madaftari/vitabu isiwe na picha yoyote
- T-shirt (fulana) ya Blue na bukta ya blue kwa ajili ya michezo.
- Tai ya rangi ya …….
- Raba jozi moja kwa ajili ya michezo
- Mkanda wa suruali mweusi

WASICHANA

- Blauzi mbili nyeupe aina ya tetroni mikono mifupi
- Sketi ya rangi ya ……. kitambaa kizito
- Viatu vyeusi vya ngozi jozi mbili
- Sweta rangi ya ……..shingo V
- Soksi nyeupe stocking pair mbili
- T-shirt (fulana) ya blue na bukta ya blue ya michezo
- Tai rangi ya ……..

- Mfuko wa vitabu au madaftari usiwe na picha yoyote
- Rangi ya hijabu ifanane na sare ya shule, kitambaa cha kichwa kishuke hadi kifuani
  Nusu kanzu ishuke hadi magotini, watakaovaa sketi ziwe ndefu. Kitambaa kiwe kilekile cha wanafunzi wengine kwa rangi na aina yake. Suruali zisiwe za kubana.

MAHITAJI YA SHULE

(a) Daftari kubwa (10) za masomo na ni vyema zote zikawa counter books
(b) Vyombo vya chakula viwe vya aluminium (visiwe vya plastic) sahani, bakuli na kijiko
(c) Rula na kifuto (raba)
(d) Kamusi ya kiingereza –Kiswahili au nyingine ya kujifunzia kiingereza atakayotumia mwanafunzi mwenyewe.

SHERIA NA KANUNI ZA SHULE HII

Shule hii inaendeshwa kwa mujibu wa sheria ya Elimu Na 25 ya mwaka 1978. Aidha inazingatia miongozo yaote inayotolewa na wizara yenye dhamana ya Elimu nchini.

Unatakiwa kuzingatiwa mabo yafuatayo ya msingi;

A. HESHIMA

i. Wanafunzi wawe na heshima kwa walimu, wafanyakazi wote, wao kwa wao na mtu mwingine yeyote anayewazidi umri.
ii. Wanafunzi hawaruhusiwi kutumia lugha mbaya wakati wowote kati yao wenyewe kwa wenyewe, kwa walimu na kwa mtu mwingine.
iii. Wanafunzi wote ni lazima washirikiane na kusaidiana na waheshimu na kuthamini kazi za aina zote.
iv. Wanafunzi wote hawaruhusiwi kufanya mambo yafuatayo:-
  (a) Kuvuta sigara, bangi, na kutumia madawa ya kulevya
  (b) Kunywa pombe
  (c) Kuvaa mavazi yasiyo ya heshima
  (d) Kugombana
v. Wanafunzi wanatakiwa kuitika mara moja na kukimbia wanakoitwa
vi. Wanafunzi wanatakiwa kuheshimu bendera ya Taifa, picha za viongozi wa serikali, wimbo wa Taifa na fedha za taifa.
vii. Wanafunzi waheshimu kumbi za mikutano, ofisi za shule, kutunza na kuthamini mali binafsi na mali ya umma.
viii. Wanafunzi wawe mfano mzuri wa hesima na tabia njema mahali popote walipo.
ix. Wanafunzi wawe kimya wakati wote wakiwa darasani wasitoke nje bila ruhusa ya mwalimu au kiongozi aliyepo.
x. Wanafunzi wanyooshe mkono juu na kusimama wanapoulizwa na kujibu maswali
xi. Uhusiano kati ya mvulana na msichana uwe wa kimasomo tu.
xii. Ni lazima wanafunzi wote wahudhurie vipindi vyote vya masomo ndani na nje ya darasa.
xiii. Wanafunzi wote lazima wahudhurie kazi zote za mikono
xiv. Wanafunzi wote ni lazima wahudhurie mikutano yote ya shule kama baraza la shule, ukaguzi wa usafi na kupandisha bendera ya Taifa.
xv. Kwa kuzingatia sheria ndogo ya mahuhurio ya lazima katika shule za sekondari wilayani Hanang-mwanafunzi atakayekosa/kuacha shule BILA SABABU YA MSINGI pamoja na **MZAZI/MLEZI** atakae sababisha mwanafunzi kuacha shule/masomo atachukuliwa hatua za **KISHERIA KWA KUZINGATIA SHERIA NDOGO HIYO**

B. KUWAHI

(i) Wanafunzi wote ni lazima wawahi katika shughuli zote za shule kama zilivyo pangwa kwa ratiba ya kila siku, kama vile vipindi vya darasani na nje ya darasa, wakati wa zamu, kurudi shuleni baada likizo n.k

(ii) Wanafunzi ni lazima wawahi haraka wanaposikia wito wa dharura

C. SARE ZA SHULE

(i) Ni lazima wanafunzi wote wavae sare ya shule wakati wote wa;-

(a) Masomo ya darasani
(b) Wanapotoka nje kwa shughuli za kishule
(c) Mhadhara wa shule (baraza)
(d) Wanapokwenda hospitali
(e) Maandamano rasmi
(f) Wanapokuja shuleni na kurudi nyumbani jioni
(g) Kofia, kiatu cha ghorofa na mapambo yoyote haviruhusiwi kuvaliwa na sare
(h) Usafi wa sare na mavazi yote yaliyoruhusiwa kuvaliwa shuleni ni lazima uzingatiwe kwa kila hali.
(i) Wanafunzi wanaruhusiwa kuvaa buti nyeusi za mvua (rainboots) wakati wa mvua tu. Usafi wa buti hizi ni muhimu kuzingatiwa

D. MIPAKA YA SHULE

(i) Wanafunzi hawaruhusiwi kutoka nje ya shule bila kibali/ruhusa maalum na warudi kwa saa zilizoruhusuwa/pangwa

(ii) Wanafunzi hawaruhusiwi kutembelea sehemu zifuatazo bila ya kibali maalum;-

(a) Ofisi za shule
(b) Nyumba za walimu na wafanyakazi wasio walimu
(c) Vilabu vya pombe
(d) Nyumba za starehe
(e) Nyumba za kulala wageni

E. USAFI

(i) kila mwanafunzi lazima azingatie usafi wa vifaa vyote anavyotumia hapa shuleni, usafi wake binafsi kama vile mwili n.k

(ii) kila mwanafunzi lazima awajibike kwenye usafi wa mazingira ya shule, ni marufuku kutupa makaratasi hovyo. Pia ni marufuku kupita njia za vichochoro, kila mwanafunzi lazima atunze bustani za maua kwa kila hali n.k.

F. MAKOSA YANAYOWEZA KUSABABISHA MWANAFUNZI KUFUKUZWA SHULENI

1. Wizi
2. Uasherati, ushoga, na usagaji
3. Ubakaji
4. Ulevi na matumizi ya madawa ya kulevya
5. Makosa ya jinai
6. Kupigana na kupiga
7. Kuharibu kwa makusudi mali ya umma
8. Kudharau bendera ya Taifa
9. Kuolewa au kuowa/kuoana
10. Kupata mimba/kusababisha mimba ndani na nje ya shule
11. Kugoma, kuchochea na kuongoza au kuvuruga amani na usalama wa shule au watu.
12. Kukataa adhabu kwa makusudi
13. Wanafunzi kuwa na simu za mkononi

1. **MUHIMU (TANBIHI)**

Adhabu kwa uvunjaji wa sheria za shule zitatolewa na baraza la walimu, Bodi ya shule na vyombo vingine vinavyohusika. Pia nyuma ya fomu hii imeambatanishwa fomu ya vipimo vya kitabibu ambayo mwanao atapaswa kupimwa na kujaziwa fomu hiyo na daktari za zahanati au hospitali ya serikali na kisha fomu hiyo aje nayo mwanao wakati wa kuripo shuleni.

2. Vilevile nyuma ya fomu hii kuna fomu kuna fomu ya kiapo cha mzazi/mlezi na mwanafunzi ambavyo vyote kwa pamoja vinatakiwa vijazwe kikamilifu na kuwasilishwa shuleni wakati mwanafunzi anaripoti shuleni.

Nakutania utekelezaji mwema

…….

SHULE YA SEKONDARI CHIEF GIDOBAT
S. L. P 167,
KATESH-HANANG,
MANYARA.

KIAPO CHA MZAZI/MLEZI

Mimi…….nakubali kuwajibika juu ya mwanafunzi ……..na kwamba sitakuwa sababu ya yeye kushindwa kuendelea na masomo.

Jina_____ Sahihi _____

Tarehe _____

KIAPO CHA MWANAFUNZI

Mimi ……..nimesoma na kuelewa sheria na kanuni za shule zilizo ainishwa katika fomu hii. Hivyo nipo tayari/sipo tayari kuzifuata.

Jina_____ Sahihi _____

Tarehe _____

CHIEF GIDOBAT SECONDARY SCHOOL
P.O.BOX 167 KATESH-HANANG, MANYARA
MEDICAL EXAMINATION FORM

(To be completed by a government medical officer)

Student's full name……

Age ……

Blood count (Red & White) ……

Stool examination …….

Urine analysis …….

Syphilis ……

TB test ……

Eye test ……..

Ears …….……..

Chest …… ……..

Spleen ……

Abdomen ……

Additional information eg. Physical defects/impairments infection/chronic diseases/family diseases etc ……..

……

……

I certify that the above mentioned student is fit to pursue his/her secondary school education

Signature ……. Designation ……

Station …… date ……

Stamp ……